# WADAU WAKUTANA KUJADILI MKAKATI WA USAJILI WA MATUKIO MUHIMU YA BINADAMU NA TAKWIMU



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na sheria Bw. Amon Mpanju akiwa katika picha ya kumbukumbu na wadau wa Kitaifa na Kimataifa ambao wamekutana hii leo Jijini Dar es salaam kujadili kuhusu Mkakati wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu pamoja na kuweka mfumo wa uratibu na mawasiliano baina ya wadau wa masuala ya usajili wa matukio hayo,anayefuata kulia kwake ni Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya RITA Bi. Victoria Lembeli anayemfuatia (kulia) ni Mjumbe wa Bodi Bi. Asha Mtwangi na kushoto kwake ni Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA Bi. Emmy Hudson na anayefuata (kushoto kwake) ni Mwakilishi kutoka shirika la Maendeleo la Kanada sekta ya Afya Dkt Madani Thiam.

Wadau wa usajili wa matukio muhimu ya Binadamu na Takwimu wamekutana kwa siku mbili jijini Dar es salaam katika warsha yenye lengo la kupata mrejesho wa maendeleo na kuweka mikakati ya utekelezaji wa Mkakati uliowekwa wa kuboresha usajili wa matukio muhimu ya Binadamu ambayo ni Vizazi, Vifo na sababu zake, Ndoa, Talaka na watoto wa Kuasili.

Akizungumza katika ufunguzi wa warsha hiyo iliyoandaliwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) kwa ushirikiano na Benki ya Dunia, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bw Amon Mpanju amesema Serikali kupitia Wizara yake inatambua kwamba inayo majukumu ya kutekeleza ikiwa ni pamoja kuwezesha Mkakati wa kitaifa wa Usajili wa Matukio muhimu ya binadamu unapita katika ngazi stahiki kabla ya kuanza kutumika na wizara tayari tumeanza kuandaa taarifa kuhusu mkakati huo na hivi karibuni itakamilika na kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi.

Vilevile Bw, Mpanju alibainisha kwamba wizara yake inaendelea na zoezi la kukusanya maoni kutoka kwa wadau kuhusu sheria mpya ya vizazi na vifo na kwamba kama kuna mdau ambaye hajapata nafasi ya kutoa maoni atumie fursa iliyotolewa.

Wakati huo huo Bw Mpanju amewahakikishia wadau wa maendeleo kuwa misaada yote ya fedha na vitendea kazi wanavyotoa kwa RITA ili kufanikisha usajili wa matukio hayo inatumika kama ulivyo kusudiwa na kuahidi kuwa Serikali itasimamia hilo. Aidha, ameipongeza RITA kwa kutekeleza mpango wa Usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika Mikoa kumi na mmoja ambapo zaidi ya asilimia themanini ya Watoto katika Mikoa hiyo wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa bila ya malipo.

"Kwa kweli RITA mnafanya vizuri na endeleeni kusimamia kazi hiyo ya usajili kwani Serikali inahitaji takwimu hizo katika kupanga maendeleo ya Taifa."alisema Bw Mpanju.

Pia alitoa wito kwa taasisi zote zinazohusika na usajili wa wananchi kuongeza kasi ya kuhakikisha mifumo yako ya tehama inaongea ili ziweze kubadilishana kwani wananchi wanosajiliwa ni walewale hivyo kusiwe na haja ya kuwasajli zaidi ya mara moja.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa Mkakati wa Usajili wa Matukio muhimu ya Biadamu, Bi Victoria Lembeli ambaye ni mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala alisema chimbuko la Mkakati huu ni kutokana na idadi ndogo ya wananchi waliosajiliwa na kupata vyeti na kuongeza kwamba baadhi ya vipengele katika mkakati huo vimeanza kutukelezwa ikiwa pamoja na kusogeza huduma karibu na wananchi sambamba na kuondoa malipo ya ada kwa watoto wa umri chini ya miaka mitano unaotekelezwa katika mikoa kumi na moja hadi sasa.

Naye Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) Bi. Emmy Hudson alisema kuwa kwa sasa taarifa zinazotokana na usajili wa vizazi,vifo,ndoa na talaka zinatumika na taasisi nyingine za serikali tofauti na hapo awali ambapo mwananchi akisajiliwa na kupatiwa cheti cha kuzaliwa anakihifadhi ndani na hakihitajiki kwa matumizi mengine lakini kwa sasa hivi vyeti vya kuzaliwa vinahitajika wakati wa kumuandikisha mtoto elimu ya msingi, Bima ya Afya,mikopo ya elimu ya juu, ajira, Vitambulisho vya Taifa pamoja na Hati ya kusafiria.

“wananchi wengi walikuwa hawaoni umuhimu wa kusajili matukio hayo lakini kwa sasa elimu inatolewa kila siku na kuongezeka kwa matumizi ya cheti cha kuzaliwa,vifo,vyeti vya

ndoa na talaka imepelekea wananchi wengi kujitokeza kwa ajili ya usajili na kupatiwa nyaraka hizo".Amesema Bi Hudson.

Ikumbukwe kuwa Mkakati huo wa Kitaifa umechanganua na kuweka mfumo thabiti wa usajili wa matukio hayo muhimu kwa manufaa ya Wananchi na Taifa katika kupanga na kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo.

Wizara,Taasisi na mashirika ya Kimataifa yaliyoshiriki mkutano huo ni Wizara ya katiba na sheria,Wizara ya Mambo ya ndani kupitia Idara ya uhamiaji, Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii jinsia Wazee na Watoto, Shirika la kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF), Serikali ya Italy kupitia ubalozi wake, Shirika la Afya Duniani WHO, CDC, Bloomberg Data for Health, Kampuni ya simu za mkononi (Tigo), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).




Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na sheria Bw. Amon Mpanju akiwasilisha hotuba ya ufunguzi wa Warsha ya siku mbili ya wadau wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu na Takwimu Jijini Dar es salaam,kulia kwake ni Kaimu Mwnyekiti wa Bodi ya Ushauri ya RITA Bi. Victoria Lembeli na kulia kwake ni Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA Bi. Emmy Hudson.